

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU TAARIFA YA UANZISHWAJI WA MCHEZO WA NGUMI, ZANZIBAR

Mheshimiwa Spika,

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana tena katika Vikao vya Baraza vinavyoendelea kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu kama Katiba inavyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika,

Kamati, inaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwnyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona ipo haja ya kuwasilishwa Taarifa hii ya Mchezo wa Ngumi mbele ya Kamati ya Ustawi wa Jamii na hatimae kupelekwa Barazani kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza kuweza kutoa maoni yao kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 44(4).

Mheshimiwa Spika,

Aidha, Kamati pia inamshukuru Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Tabia Maulid Mwita kwa juhudi alizozichukua juu ya suala zima la uanzishwaji wa Mchezo huo uliotokana na maombi yaliyotokana na Mjumbe wakati wa kuchangia Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya utangulizi huo, Kamati inakubaliana na Taarifa hii iliyowasilishwa na Serikali juu ya suala zima la Uanzishwaji wa Mchezo wa Ngumi Zanzibar, ili kutoa fursa ya kuitangaza nchi yetu Kitaifa, Kikanda pamoja na Kimataifa kupitia mchezo huo.

Mheshimiwa Spika,

Sambamba na hilo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba licha ya kukubaliana na Taarifa hiyo inaomba mambo yafuatayo yazingatiwe kabla ya kuanzishwa rasmi katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika,

Jambo la kwanza, kuwepo kwa Kanuni pamoja Miongozo itakayoelezea utaratibu utakaotumika kuhusiana na uendeshaji pamoja na usimamizi wa mchezo huo, ili kuweza kuepusha madhara yatakajitokeza kwa wananchi pamoja na Taifa kwa jumla.

Pili, kuwepo kwa mafunzo maalum ya mchezo huo yatakayofanyika ndani na nje ya nchi, ili kuwawezesha watakaosimamia mchezo huo kuweza kuuendesha kitaalamu, ili kuweza kuzalisha walimu, makocha pamoja na waamuzi wenye kukidhi vigezo vya Kitaifa na Kimataifa, kwa ajili ya kuwafundisha wananchi au vijana wetu mchezo kitaalamu.

Tatu, kuwepo kwa madaktari Bingwa watakaoweza kushughulikia wachezaji wa mchezo huo pindi pale watakapopata athari za kiafya ili kuweza kutibiwa ndani ya nchi. Kwani kama inavyofahamika kwamba Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya wataalamu hususan katika masuala ya matibabu ya mifupa pamoja na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na mapendekezo yaliyotolewa juu ya kukubaliana na Taarifa ya Uanzishwaji wa Mchezo huo, bado Kamati inaiomba Serikali ufanyike utafiti wa kina licha ya ule utafiti wa awali uliofanyika kuhusiana na athari na faida zitakazopatikana kutokana na mchezo huo, kwani Kamati imebaini utafiti huo uliofanyika haukugusa maeneo yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,

Aidha, idadi ya wananchi waliohojiwa kuhusiana na mchezo huu ambao hawazidi elfu sita, utafiti unaonesha wazee wanaozidi miaka 60 wameupinga mchezo huu. Hivyo, basi kuna umuhimu wa kutolewa elimu zaidi na utafiti uendelezwe kwa maeneo ambayo hayakuguswa na utafiti huo wa awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwatambua

Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

- | | | |
|----|------------------------------|-------------------|
| 1. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 8. | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 9. | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |


Mheshimiwa Spika,

Mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuweza kuichangia Taarifa hii kwa ajili ya kutoa maoni, ushauri pamoja na mapendekezo kuhusu uanzishwaji wa Mchezo huo katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na baadae kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante,



Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.